

TANGAZO LA AJIRA

WASCO ISOAF Tz Limited ni kampuni ya kitanzania iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria yenye makao makuu jijini Dar es Salaam na mitambo yake ya uzalishaji Mkoa wa Tabora katika wilaya ya Nzega. Kampuni inatarajia kuanza rasmi shughuli za uzalishaji kama mkandarasi wa mfumo wa Uhamishaji Joto katika mradi wa bomba la mafuta ghafla la Africa Mashariki (EACOP)

MAELEZO YA KAZI

NAFASI: MTAALAMU WA MAWASILIANO.

UTARIPOTI KWA: MENEJA WA UTENDAJI WA KIJAMII. AKIFUATA MALENGO YALIYOWEKWA NA MENEJA WA UENDESHAJI.

ENEO LA KAZI: SOJO, WILAYA YA NZEGA, MKOA WA TABORA

Lengo la kazi

- Kuwezesha mawasiliano, kuunganisha ushirikiano kati na katika idara mbalimbali, kazi na viwango vya wafanyakazi wa Wasco Isoaf katika kituo cha Mfumo wa Uondoaji Joto ardhini (TIS) eneo la Sojo, Wilaya ya Nzega.
- Kuhakikisha kwamba kuna mtiririko wa kutosha na kwa wakati wa taarifa kuhusu mwenendo wa kazi, masharti, mahitaji na maamuzi na kwamba wafanyakazi wote katika ngazi zote wanafahamishwa na wana taarifa za kutosha ili kuchangia katika utekelezaji wa kazi zao kwa ujasiri, kwa wakati na kwa usalama katika eneo la mradi.
- Kutoa shukrani miongoni mwa wafanyakazi katika eneo la mradi ya jinsi shughuli tofauti na juhudi zao mbalimbali kutokana na taaluma mbalimbali ambazo husaidia Wasco Isoaf kufanikisha malengo yake ya mkataba wa kazi kwa ufansi.

Majukumu

- Kuhamasisha wafanyakazi wafanye kazi kwa kushirikiana kama timu
- Kuonyesha njia zilizopo za mawasiliano rasmi na zisizo rasmi kwenye eneo la mradi na jinsi zinavyofanya kazi, na kwa matokeo gani.
- Kutambua mahitaji ya mawasiliano katika mikondo mbalimbali ya kazi katika eneo la mradi
- Kutambua aina ya taarifa ambazo zinahitajika kusambazwa na chanzo cha taarifa hizo, mmiliki wa kila taarifa.
- Kuanzisha njia ya mawasiliano ya idara za ndani
- Kuanzisha njia za mawasiliano za kawaida, zinazoendelea, zilizowima na za mlalo kati ya vipengele tofauti vya utendaji kazi katika eneo la mradi.
- Kuweka wazi mawasiliano yaliyoidhinishwa, mtiririko wa

taarifa na muingiliano kwa wafanyakazi wote.

- Kuanzisha njia zilizowazi kwa wafanyakazi ili waweza kupata taarifa za utaratibu, maamuzi, itifaki, taarifa kuhusu matukio, malengo ya Wasco Isoaf na maendeleo ya kazi ikiwa ni pamoja na kutambua watu muhimu wa kuwasiliana nao ambao wanaweza kufikiwa kuhusiana na aina mahususi za taarifa.
- Kuanzisha matukio ya mara kwa mara ya kubadilishana taarifa ana kwa ana na mawazo kati ya viwango tofauti vya wafanyakazi, kufanyia kazi vipengele tofauti vya Wasco Isoaf.
- Kuendeleza mawasiliano katika eneo la mradi kwa kuzingatia taarifa zilizo wazi, kwa wakati, na sahihi na ahakikishe kuwa taarifa na ujumbe umewekwa wazi kwa utaratibu na kwa uthabiti kwa wafanyakazi wote.
- Kuanzisha jukwaa kwa ajili ya wafanyakazi kupata mrejesho kutoka kwa uongozi wa mradi na uongozi kupata taarifa kutoka kwa wafanyakazi
- Kuanzisha jukwaa la matukio ya mara kwa mara ya kitamaduni ili kukuzua uelewa wa msuala ya kitamaduni kwa wafanyakazi.
- Kuhudumia mifumo ya mawasiliano ili kuhakikisha inafanya kazi ipasavyo; kurekebisha na kuifanyia maboresho ikiwa itashindwa kuwezesha mtiririko wa taarifa na maoni ya wafanyakazi.

Sifa, uwezo na uzoefu

- Uwezo wa kuwasiliana vyema
- Uwezo wa kuelewa mazingira ya kiufundi, uhandisi, viwanda, ujenzi na kutafsiri maudhui ya kiufundi katika taarifa zinazoelweka na zinazoweza kufikiwa.
- Uzoefu wa kufanya kazi katika kuongoza na kuwezesha michakato inayowezesha na kuimarisha maelewano kati ya timu za kitaifa na za tamaduni tofauti zinazofanya kazi katika muktadha wa viwanda, ujenzi na/au uzalishaji.
- Uwezo wa kuwa kama wakala, kusimamia maadili na kutambuliwa kati ya wafanyakazi tofauti.
- Awe anafahamu kikamilifu Kiingereza na Kiswahili na ikiwezekana lugha ya tatu.
- Awe mwadilifu na mwenye maadili ya kazi

Kiunganishi kati ya

- Wasimamizi wa eneo la mradi
- Idara zote/ wasimamizi wa kazi au wawakilishi wa eneo la mradi.